TANGAZO LA SERIKALI Na. 789 la tarehe. 6/9/2024

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 9(1) na (2))*

NOTISI YA KUONGEZA ENEO LA KUTOA HUDUMA LA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA GEITA YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikama kama Notisi ya Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Geita ya Mwaka 2024.

Kuongezwa eneo la huduma

2.-(1) Eneo la huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Geita linaongezwa kujumuisha maeneo yaliyoainishwa katika Jedwali.

(2) Chombo chochote ngazi ya jamii au chombo kilicho sajiliwa, kabla ya kuanza kutumika kwa Notisi hii, kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira katika eneo la huduma linaloongezwa, kitaacha kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira katika eneo hilo mara tu baada ya Notisi hii kuanza kutumika.

(3) Haki, wajibu, masharti ya ajira ya watumishi, mali, madeni na masuala mengine yanayohusiana yaliyotolewa au yanayotekelezwa na chombo chochote kilichorejewa katika aya ndogo ya (2) yatabaki chini ya himaya ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Geita.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2(1))*

| JINA LA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA | ENEO LA HUDUMA LINALOONGEZWA |
|---|---|
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Geita. | Kata zifuatazo: Ludete,Chigunga,Bukondo,Nyamigota, Katoro, Chikobe, Buseresere na Nyakagomba |

Dodoma,
13 Agosti, 2024

JUMAA HAMIDU AWESO,
*Waziri wa Maji*